# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI, NAM. 15 YA 1986**

3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 2.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2006**

5. Kusomwa.

6. Marekebisho ya kifungu cha 25

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005.**

7. Kusomwa.

8. Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI, NAM. 7 YA 2013

9. Kusomwa.

10. Kufuta vifungu vya 33, 34 na 35.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013

11. Kusomwa.

12. Marekebisho ya kifungu cha 238.

**SHERIA NAM. 10 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

22 Disemba, 2022

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanzia kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii, zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI, NAM. 15 YA 1986

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Nam. 15 ya 1986 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**4.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2) na badala yake kuweka kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Sheria hii haitotumika kwa wafanyakazi walioajiriwa katika Taasisi za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania zilizopo Zanzibar na wafanyakazi walioajiriwa katika sekta ya umma au binafsi Zanzibar ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar";

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Wafanyakazi wote katika sekta za umma na binafsi ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar watalipwa fao la kuumia kazini kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na Kanuni zake:

(c) kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (3) na kuwa kifungu kidogo cha (4).

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2006

Kusomwa.

**5.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar, Nam. 1 ya 2006 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 25.

**6.** Kifungu cha 25 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(6) Mdaawa katika rufaa, katika hatua yoyote ya mwenendo kabla ya hukumu haijatolewa na Bodi au Baraza vyovyote itakavyokuwa, anaweza kuomba rufaa imalizike kwa makubaliano ya pande mbili.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, Bodi au Baraza:

(a) litawataka wadaawa kutoa taarifa ya matokeo ya makubaliano ndani ya muda uliyoainishwa, na Bodi au Baraza litatoa amri ya mwisho kuhusiana na makubaliano hayo;

(b) litatoa amri ya mwisho baada ya kuwasilishwa makubaliano yaliyosainiwa na wadaawa wote; na

(c) halitoshughulikia jambo ambalo limetatuliwa kwa makubaliano na wadaawa chini ya masharti ya kifungu hiki."

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

Kusomwa.

**7.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

**8.** Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (d) mara baada ya aya ya (c) katika kipengele cha 2 kama ifuatavyo:

"(d) fao la kuumia kazini asilimia moja".

(b) kufuta neno "kumi na tatu" na badala yake kuweka neno "kumi na nne" katika aya ya (b) ya kipengele cha 3.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI, NAM. 7 YA 2013

Kusomwa.

**9.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, Nam. 7 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta vifungu vya 33, 34 na 35.

**10.** Vifungu vya 33, 34 na 35 vya Sheria Mama vinafutwa.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013

Kusomwa.

**11.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Makampuni, Nam. 15 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 238.

**12.** Kifungu cha 238 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 13 Disemba, 2022.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***

***Zanzibar.***